


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



TAARIFA YA MAENDELEO YA ELIMU KWA MKOA WA Mtwara 2017

Imetayarishwa Na:

**Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,
S.L.P 544,
MTWARA.**

Simu Na: 0232333014/2334065

Fax Na: 023 2333014/2333194

Email: ras@mtwara.go.tz

mtwara.reo@gmail.com

UTANGULIZI

Mkoa wa Mtwara una jumla ya Wilaya 5, Halmashauri 9, Tarafa 27, Kata 191, Mitaa 179, Vijiji 792 na Vitongoji 3456. Aidha Mkoa una jumla ya majimbo ya uchaguzi 10

Mamlaka zote hizi zina wajibu wa kusimamia shughuli za maendeleo katika ngazi zao husika ikiwemo na suala zima la Elimu.

HALI YA MAAENDELEO YA ELIMU

ELIMU YA AWALI

Mkoa una jumla ya shule za Msingi 659, kati ya hizo shule 653 ni za Serikali na shule 6 ni shule binafsi. Katika shule za Serikali 653, shule 643 zina madarasa ya awali na shule 10 hazijawa na madarasa hayo ya awali. (4 za Halmashauri ya Wilaya ya Masasi na 6 Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba)

UANDIKISHAJI ELIMU YA AWALI

2014		2015		2016		2017	
LENGO	HALISI	LENGO	HALISI	LENGO	HALISI	LENGO	HALISI
40,057	35,232	38,717	34,870	36,403	39,149	48,067	
	88%		90%		108%		

UANDIKISHAJI ELIMU YA MSINGI

2014		2015		2016		2017	
LENGO	HALISI	LENGO	HALISI	LENGO	HALISI	LENGO	HALISI
40,783	37,517	37,609	37,906	35,944	51,756	44,149	
	92%		103%		144%		

UHITIMU

	2014	2015	2016
WALIOMALIZA STD VII	69.5%	69.2%	69%
MDONDOKO	29.5%	30.6%	31%

MIMBA

	2014	2015	2016
WALIOPATA MIMBA	12	10	24

UFAULU

S/Na.	MWAKA	WALIOFANYA MTHANI			WALIOFAULU			%	NAFASI KITAIFA
		WAV	WAS	JML	WAV	WAS	JML		
1	2007	12409	11963	24372	6452	6220	12672	52.1	17/21
2	2008	14905	14375	29280	7933	5258	13191	45.1	16/21
3	2009	14329	14796	29125	7343	5500	12843	44.1	18/21
4	2010	12050	12974	25024	6418	5530	11948	47.7	14/21
5	2011	14827	16968	31795	8078	7869	15947	50.2	16/21
6	2012	12090	14197	26287	3213	2682	5895	22.4	20/21
7	2013	12324	14423	26767	6066	5891	11957	44.7	18/21
8	2014	11117	13893	25015	7227	8381	15608	62.0	8/21
9	2015	10304	12598	22902	7215	8455	15670	68.42	12/25
10	2016	10895	12966	23861	6520	6917	13437	56.31	25/26

MIUNDOMBINU

Halmashauri	Vyumba vya madarasa			Nyumba za walimu			Matundu ya vyoo		
	Mahitaji	Vilivyopo	Upungufu	Mahitaji	zilizopo	Upungufu	Mahitaji	Vilivyopo	Upungufu
Mtwara M	438	239	199	452	52	400	839	327	512
Mtwara V	1300	783	517	1121	265	856	2024	1293	731
Tandahimba	1175	706	469	1102	239	863	2131	832	1299
Newala	1140	713	427	1147	258	889	1686	840	846
Masaki V	1332	722	610	1332	399	933	2107	984	1123
Masaki Mji	468	236	232	559	73	486	754	421	333
Nanyumbu	712	458	254	1013	344	669	1594	556	1038
Jumla	6565	3857	2708	6726	1630	5096	11135	5253	5882

(i) Madawati

Upungufu wa madawati ulikuwa 18,528, yaliyotengenezwa 24,113 (130%) na kuwa na ziada ya madawati 5,5,85.

IDADI YA WALIMU - Idadi ya walimu ikilinganishwa na wanafunzi

Halmashauri	Idadi ya wanafunzi Darasa la I-VII	Mahitaji ya walimu	Walimu waliopo	Upungufu wa walimu	% ya upungufu	Uwiano kati ya walimu na wanafunzi
Mtwara M	20,854	460	458	2	0.4	1:45
Mtwara V	30,243	1332	1095	237	18	1:32
Nanyamba Mji	27,175	545	456	89	16	1:48
Tandahimba	47,302	1340	1111	229	17	1:32
Newala	24,116	602	448	154	25	1:53
Newala Mji	19,807	495	410	85	17	1:40
Masasi V	46,142	1331	1049	282	21	1:44
Masasi Mji	18,449	422	405	17	4	1:42
Nanyumbu	30,854	1000	688	312	31.2	1:41
Jumla	264,942	7527	6120	1470	19.52	1:43

ELIMU YA SEKONDARI

Mkoa una jumla ya shule za sekondari 147 na kati ya hizo shule 135 ni za Serikali na 12 binafsi. Jumla ya wanafunzi kwa shule zote ni 40,272.

Udahili na kuripoti shule kidato cha I mwaka 2015 (Mwezi Machi,) kulinganisha na mwaka 2016 (Mwezi Machi,)

H/SHAURI	2015						2016						ASILIMIA YA WALIORIPOTI	
	WALIODAHILIWA			WALIORIPOTI			WALIODAHILIWA			WALIORIPOTI			2015	2016
	WV	WS	JML	WV	WS	JML	WV	WS	JML	WV	WS	JML		
Mtwara (M)	563	565	1128	501	520	1021	634	771	1405	632	768	1400	90.5	99.6
Mtwara (V)	1498	1776	3274	1276	1381	2657	753	973	1726	733	911	1644	81.2	95.2
Newala DC	1102	1270	2372	887	948	1835	674	730	1404	669	715	1384	77.0	98.6
Tandahimba	1531	1973	3504	1107	1271	2378	1495	1792	3287	1456	1739	3195	68.0	97.2
Masasi DC	1303	1497	2800	922	980	1902	1116	1307	2423	1064	1227	2291	67.9	94.6
Nanyumbu	700	733	1433	503	503	1006	633	740	1373	607	696	1303	70.2	94.6
Masasi Mji	530	567	1097	392	419	811	496	472	968	462	438	900	73.9	93.0
Nanyamba Mji	0	0	0	0	0	0	734	826	1560	714	790	1504	-	96.4
Newala Mji	0	0	0	0	0	0	550	664	1214	547	657	1204	-	99.2
JUMLA	7227	8381	15608	5588	602	1161	7085	8275	1536	6884	7941	1482	74.3	96.5

MIMBA

	2014	2015	2016
WALIOPATA MIMBA	10	45	119

UFAULU - ELIMU YA SEKONDARI

		FORM II	FROM IV	FORM VI
1	2011	57%	38%	94.5%
2	2012	62%	21.7%	93%
3	2013	65	47%	96%
4	2014	77%	65%	96.5%
5	2015	67.7%	56.5%	93.5%
6	2016	66.5%	-	99%

MIUNDOMBINU - Hali ya miundombinu shule za Sekondari

Halmashauri	Madarasa			Nyumba za walimu			Matundu ya vyoo		
	Mahitaji	Vilivyopo	Upungufu	Mahitaji	Vilivyopo	upungufu	Mahitaji	Vilivyopo	Upungufu
Mtwara M	217	176	41	352	59	293	284	196	88
Mtwara V	128	91	37	325	34	291	224	135	89
Nanyamba Mji	117	99	27	169	37	132	156	79	77
Tandahimba	286	210	76	464	81	383	518	262	256
Newala	260	206	54	353	77	276	420	239	181
Masasi Mji	139	105	34	224	49	175	468	135	333
Masasi V	185	248	0	423	132	291	285	324	0
Nanyumbu	145	88	57	341	41	300	255	101	154
Jumla	1477	1223	326	2651	510	2141	2610	1471	1178

Ukamilishaji wa ujenzi wa maabara tatu katika kila shule ya sekondari Mkoa wa Mtwara

Halmashauri	Idadi ya Shule za sekondari	Mahitaji ya Maabara	HATUA ZA UTEKELEZAJI				
			Maabara Zilizokami lika na Zinatumi a Kufundishi a	Maabara Zilizofikia Hatua ya Kuweka Miundombinu ya Gesi, Maji na Umeme	Maabara zinazo fanyiwa Umalizia ji	Maabara Zilizofikia hatua ya Gebo/Lint a	Jumla
Mtwara (M)	13	39	15	24	0	0	39
Mtwara (V)	11	33	0	10	16	7	33
Tandahimba	28	84	0	6	77	1	84
Newala Dc	15	45	5	40	0	0	45
Newala TC	11	33	9	24	0	0	33
Masasi (V)	26	78	12	65	1	0	78
Nanyumbu	12	36	5	10	13	8	36
Masasi Mji	9	27	7	18	2	0	27
Nanyamba	10	30	2	2	26	0	30
Jumla Kuu	135	405	55	199	135	16	405

(ii) Madawati

Upungufu wa madawati ulikuwa 10,262 yaliyotengenezwa 10,590 (100.53%) na kuwa na ziada ya madawati 228

IDADI YA WALIMU

Mahitaji ya walimu

Halmashauri	Walimu wa masomo ya sayansi na hisabati				Walimu wa masomo ya sanaa			% ya waliopo	Walimu wa masomo ya Biashara			
	Mahitaji	Waliopo	Upungufu	%	Mah	Wal	Up/ziada		Mah	Wal	Up	%
Mtwara (M)	120	73	47	39	238	334	+96	140	25	5	20	80
Mtwara (R)	144	54	90	167	144	286	+162	199	6	2	4	67
Nanyamba TC	87	25	62	54	249	205	-44	82	10	2	8	80
Tandahimba	226	74	152	67	236	368	+132	156	8	4	4	50
Newala	220	90	130	59	260	337	+177	130	10	4	6	60
Masasi(DC)	234	101	133	57	276	314	+138	114	10	8	2	20
Masasi(TC)	89	29	60	67	138	189	+51	137	2	2	0	0
Nanyumbu	132	42	90	68	205	279	+74	136	8	20	0	0
Jumla	1231	469	762	62	1746	2312	786	132	69	45	24	30

UPANUZI WA SHULE ZA KIDATO CHA TANO

Mahitaji ya shule za “A Level” ni 27 (Idadi ya Tarafa); zilizopo 8 na upungufu 19. Kwa kuanzia imeagizwa angalau kila Halmashauri iwe na shule moja yenye *A level*. Halmashauri zenye shule hizo ni zifuatazo:-

Halmashauri zenye shule za “A Level”

Na.	Jina la Halmashauri	Jina la shule
1	Mtwara Manispaa	Mtwara Ufundi Mtwara wasichana
2	Masasi	Ndanda
3	Masasi Mji	Masasi Wasichana
4	Newala	Nangwanda Mnyambe
5	Newala Mji	Kiuta
6	Tandahimba	Tandahimba
Jumla ya shule		8

Shule za sekondari za Chidya (wavulana) na Ndwika (wasichana) ambazo zilikuwa za kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha I-IV kwa mwaka huu Wizara

yenye dhamana ya uendeshaji wa elimu (OR-TAMISEMI) imezuia kupeleka kidato cha kwanza katika shule hizo badala yake zitachukua wanafunzi wa kidato cha tano.

Hali hii imetokana na ongezeko la wanafunzi ya wenye sifa ya kujiunga na masomo ya A level kukosa nafasi. Halmashauri ya Mtwara imeahidi shule yake ya sekondari ya Nanguruwe itachukua wanafunzi wa kidato cha tano mwaka huu 2017.

Wito ni kwa kila halmashauri kujitahidi kuwa na shule hizo au kuongeza nafasi kwa shule zilizopo.

SHULE 9 ZA MKOA WA Mtwara ZILIZO KATIKA KUNDI LA UFAULU DUNI KITAIFA KIDATO CHA PILI

Jina la shule	Halmashauri	Kata	Idadi ya Walimu		Ufaulu					JUMLA
			Sanaa	Sayansi	Div I	Div II	Div III	Div IV	Div 0	
Chingungwe	Tandahimba	Chingungwe	8	0	0	0	1	15	27	43
Malocho	Newala Mji	Nanguruwe	13	1	0	0	0	23	36	59
Chanikanguo	Masasi DC	Mpindimbi	10	2	0	1	2	17	39	59
Naputa	Tandahimba	Naputa	13	1	0	0	2	40	66	108
Mtiniko	Nanyamba	Mtimbwilimbwi	19	1	0	3	3	49	89	144
Michiga	Nanyumbu	Michiga	23	2	0	0	1	29	38	68
Msimbati	Mtwara V	Msimbati	18	2	0	0	0	28	28	56
Salama	Tandahimba	Chingungwe	12	0	0	1	0	26	29	56
Lukokoda	Tandahimba	Lukokoda	9	2	0	0	0	20	19	39

CHANGAMOTO ZILIZOPO

1. UDANGANYIFU KWENYE MITIHANI YA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI

Mwaka 2015 Mkoa ulianza kupokea wanafunzi waliohitimu mwaka 2014 na kufanya vizuri sana na Mkoa kushika nafasi ya 8 Kitaifa, wakirudishwa toka shule maalum za Kilakala 14, Msalato 1, Mzumbe 1 kwa kushindwa kabisa kumudu masomo ya sekondari.

Jambo hili pamoja na kuweka mikakati ya kutoa elimu bora Mkoani, ilitulazimu kuiboresha usimamizi wa mitihani mwaka 2016.

Katika kufanya hayo tulibani kuna udanganyifu ulikuwa unafanyika kwa kuwa matokeo ya darasa la saba 2016 yameonyesha wazi kuna shule zaidi ya 63 ufaulu umeshuka kwa zaidi ya 50%.

Zipo baadhi ya Halmashauri ambazo zilifanya vizuri 2015 na kufanya vibaya sana mwaka 2016 wakati watu ni wale wale na mazingira ni yale yale.

Aidha kulikuwa na matukio ya kukamata wasimamizi wakitaka kufanya udanganyifu na kushuka sana kwa ufaulu wa ujumla kwa Halmashauri.

Na.	JINA LA HALMASHAURI	NAFASI KITAIFA 2015	NAFASI KITAIFA 2016
1	Mtwara Vijijini	16	128
2	Mtwara Manispaa	41	85
3	Newala	71	162
4	Tandahimba	53	114

Haya ni matokeo ya darasa la saba ambao tunategemea wakajiunge na sekondari na kufanya vizuri katika masomo yao. Msingi unapokuwa mbovu lazima upate matokeo mabovu.

- **KUWEPO KWA UTORO**

- Hili nalo linachangia kwa kiasi kikubwa sana maendeleo mabaya ya elimu kwa watoto wetu. Mfano kwa miaka mitatu mfululizo wastani wa watoto wanaomaliza mafunzo ni 65% hili ni tatizo.

- **UWAJIBIKAJI DUNI WA WAKUU WA SHULE NA WALIMU**

- Walimu na hasa Wakuu wa shule waliopewa dhamana ya uongozi kutosimamia walimu na wanafunzi waliokabidhiwa

- **WAKAGUZI WA ELIMU KUTOTIMIZA WAJIBU WAO**

- Wapo wakaguzi wa shughuli za shule kwa ngazi zao kama idara ya ukaguzi, Maafisa Elimu, WEO, VEO, MEO nao wanafanya kazi kwa mazoea.

- **MUAMKO DUNI WA WAZAZI NA WALEZI**

- Nao wana mchango mkubwa kwa ufaulu wa wanafunzi kwa kuwapa malezi mema na huduma zote muhimu ikiwemo upendo na ufuatiliaji.

- **UMBALI WA SHULE NA MAKAZI**

- Zipo shule chache kati ya hizi ziko mbali kidogo kati ya km2 hadi 5 kutoka Makazi ya watu, hili nalo ni tatizo hasa ukizingatia hakuna Chakula kinachotolewa shuleni.

SULUHISHO LA MATATIZO HAYA 2016/17 NA KUENDELEA

KUSHIRIKISHA WADAU MBALIMBALI WA ELIMU NGAZI ZOTE MKOANI

Jambo hili limeanza kufanyika na hata tarehe 14 Januari, tulikuwa na kikao cha wadau na yapo mambo mazuri tulikubaliana kuyatekeleza kama ifuatavyo:

- Kuweka kwenye bajeti za Halmashauri fedha za kutosha kwa ajili ya kuimarisha Miundombinu, ukaguzi, mlo na motisha kwa watakaofanya vizuri.
- Kuwashirikisha wadau mbalimbali wakiwemo wazazi na walezi katika kudhibiti utoro na mimba
- Kushirikisha vyombo vya dola hasa mahakama katika kuhuisha mipango yetu.
- Kuchukua hatua kali mara moja kwa yeyote atakayeonekana kutotimiza wajibu wake
- Kutumia vyombo vya habari hasa radio za ndani kuhamsisha Elimu
- Kila Wilaya kuwa na mikakati wake kulingana na mazingira yake na kuuwakilisha Mkoani kabla ya tarehe 30 Januari, 2017
- Kuwepo na vikao vya wadau angalau mara mbili kwa mwaka
- Vikao vyote vya Serikali ngazi zote suala la Elimu liwe suala la kipaumbele